

# **Je, wanafanya kazi kwa ajili yetu? Mambo nane kuhusu wabunge Tanzania**



## **1. Utangulizi**

Bunge la Tanzania ni moja ya taasisi muhimu sana nchini. Umuhimu wa Bunge unadhihirishwa na mgawo wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Bunge. Kwa mwaka wa fedha 2009/10 kiasi cha bajeti kilichotengwa kwa ajii ya Bunge ni Sh bilioni 62. Kwa kuwa kuna jumla ya wabunge 320, kiasi hiki ni wastani Sh milioni 194 kwa kila Mbunge.

Wabunge wengi (231) wanachaguliwa na wapiga kura kwenye majimbo yao, lakini idadi kubwa (88), au karibu asilimia 28 ya wabunge wote, ni wa kuteuliwa: wabunge 75 ni wa viti maalum na wabunge 5 wawakilishi kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Kwa nyongeza Bunge linajumuisha pia wabunge 8 wa kuteuliwa na Rais mmoja wao akiwa ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Moja ya kazi zake kuu ni kusimamia utendaji wa Serikali. Bunge linahakikisha kwamba nchi inaendeshwa vizuri, huduma zinatolewa kiusahihi kwa wananchi, na kwamba fedha za wananchi zinatumika vizuri na zinatolewa maelezo. Wabunge wanaweza kuiwajibisha Serikali kwa kufanya ushiriki wa aina tatu: wabunge wanaweza kuuliza maswali ya msingi, wanaweza kuuliza maswali ya nyongeza na wanaweza kutoa michango wakati wa mjadala.

Muhtasari huu unapima utendaji wa wabunge kwa kuzingatia namna walivyoshiriki katika vikao vya Bunge. Kipindi kilichopitiwa ni vikao 17 vya Bunge kuanzia mwaka 2005 hadi 2009 (kikao cha 18 kilichoanza tarehe 26 Januari 2010 hakijajumuishwa).



Muhtasari huu umeandaliwa na Uwazi InfoShop iliyopo Twaweza/Hivos Tanzania.

Uwazi, S.L.P38342, Dar es Salaam, Tanzania.  
Simu +255 22 266 4301. Faksi +255 22 266 4308.  
Email: [info@uwazi.org](mailto:info@uwazi.org). Web: [www.uwazi.org](http://www.uwazi.org)

## 2. Mambo nane kuhusu Bunge la Tanzania

Wabunge wote wana nafasi sawa ya kuuliza maswali au kutoa mchango, lakini Mawaziri wa Serikali kwa kawaida hawafanyi hivyo. Maswali ni nyenzo kuu ya wabunge kuchunguza kwa makini shughuli za Serikali. Maswali ya msingi yanawekwa kwenye maandishi na kuwasilishwa Serikalini kabla ya kikao husika cha Bunge. Wakati wa kikao cha Bunge, serikali (hasa waziri husika) anatoa majibu ya maswali hayo. Maswali ya nyongeza ni maswali ya ziada yanayoulizwa na wabunge kufuatia majibu ya serikali ya swali la msingi. Maswali haya yanaulizwa wakati wa mjadala na yanajibowi hapo hapo. Michango ni maoni yanayotolewa na wabunge Bungeni ambayo sio maswali rasmi. Michango hii inaweza kuwa ni maoni ya kawaida au hoja inayotolewa kipindi cha mjadala au maoni juu ya muswada uliopendekezwa kujadiliwa.

Muhtasari huu unawasilisha mambo nane muhimu yaliyochambuliwa kutoka kwenye taarifa za Bunge zilizochukuliwa kwenye Mfumo wa Mtando wa Taarifa za Bunge kwa Umma (POLIS) kwenye tovuti ya Bunge la Tanzania (<http://www.bunge.go.tz>) kama zilivyopatikana mwezi Januari 2010. Data kamili na mpangilio wa ngazi za ushiriki wa wabunge wote umewasilishwa kwenye Kiambatisho namba 1.

Ukweli wa 1: Bunge la Tanzania liko wazi

Bunge la Tanzania linafanya vizuri kuhakikisha taarifa zinapatikana kwa wananchi. Tovuti ya Bunge inapatikana na kutumiwa kiurahisi, ina taarifa za hivi karibuni na ina taarifa husika nyingi na muhimu. Katika nyanja nyingi inadhihirisha nia ya dhati na jitihada za Mheshimiwa Samuel Sitta, Spika wa Bunge, ambaye anaeleza kwenye tovuti ya Bunge kuwa:


*“Bunge la Tanzania linahakikisha linaingiza taarifa za sasa na kurekebisha zilizomo kwenye POLIS ili kuhakikisha wadau wote na wananchi kwa ujumla wanapata taarifa za kutosha za shughuli za Bunge. Zaidi ya hilo, ni makusudio ya Bunge kurekebisha na kuufanya mfumo huu kuwa chanzo cha uhakika cha taarifa za Bunge.” (tafsiri yetu)*

Taarifa zote katika muhtasari huu, zikiwemo taarifa za bajeti zilizonukuliwa kwenye utangulizi, zilichukuliwa kiurahisi tu kwenye tovuti ya Bunge.

## **Ukweli wa 2: CCM ni chama Kinachochangia zaidi Bungeni**

Tangu uchaguzi wa mwaka 2005, idadi ya ushiriki wa wabunge kwenye mijadala ya vikao vya Bunge ni 19,039. Ndani ya idadi hiyo maswali ya msingi yalikuwa 3,922 na maswali ya nyongeza yalikuwa 5,882. Jumla ya michango ya wabunge ilikuwa 9,235.

**Mchoro 1: Ushiriki Bungeni ki-chama**




Chanzo: Tovuti ya Bunge la Tanzania ([www.bunge.go.tz](http://www.bunge.go.tz))

Katika idadi yote ya ushiriki wa wabunge Bungeni, michango ya ushiriki 15,410 ilitoka kwa wabunge wa CCM wakati michango ya ushiriki 2,150 ilitolewa na wabunge wa CUF na michango ya ushiriki 1,337 ilitolewa na wabunge wa CHADEMA. UDP chama chenye mbunge mmoja Bungeni kilitoa michango ya ushiriki 142. Mchangano mkubwa wa CCM ni wazi kuwa unatokana na idadi kubwa ya wabunge iliyo nao. Wabunge 277 (au 87% ya wabunge wote) ni wa CCM, ukilinganisha na wabunge 31 (10%) wa CUF, wabunge 11 (3%) wa CHADEMA, na 1 (0.3%) wa UDP.

## **Ukweli wa 3: Wabunge wa upinzani wanashiriki zaidi kuliko wa chama tawala**

Mchoro namba 2 unaonesha matokeo ya utendaji wa vyama tofauti vilipopimwa idadi ya ushiriki kwa kila mbunge. Kwa kuangalia uchangiaji wa maswali ya msingi, CHADEMA inashika nafasi ya kwanza ikiwa na wastani wa maswali ya msingi 19 kwa kila mbunge. CHADEMA pia inashika nafasi ya kwanza kwenye maswali ya nyongeza ikiwa na wastani wa maswali 36 ya nyongeza kwa kila mbunge. UDP (chenye mbunge 1) kinashika nafasi ya juu kabisa kwenye eneo la kutoa michango Bungeni. Chama tawala(CCM) kinashika nafasi ya mwisho katika kila aina ya ushiriki Bungeni kikiwa na wastani wa maswali ya msingi 12, maswali ya nyongeza 17 na wastani wa michango 26 kwa kila mbunge.

## Mchoro 2: Wastani wa idadi ya maswali na michango kwa kila kila mbunge, ki-chama




Chanzo: Tovuti ya Bunge la Tanzania ([www.bunge.go.tz](http://www.bunge.go.tz))

## Ukweli wa 4: Wabunge waliochaguliwa wanachangia zaidi kuliko walioteuliwa

Katika nyanja zote, wabunge wa kuchaguliwa wamewazidi kuitendaji wabunge wa kuteuliwa, isipokuwa wabunge wa viti maalumu wanautendaji mzuri zaidi kwenye kutoa michango Bungeni. Wabunge kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar na wale walioteuliwa na Rais wanaushiriki mdogo sana Bungeni.

## Mchoro 3: Idadi ya ushiriki wa wabunge, kwa-aina ya ubunge




Chanzo: Tovuti ya Bunge la Tanzania ([www.bunge.go.tz](http://www.bunge.go.tz))

## Ukweli wa 5: Wabunge wanaume wanashiriki zaidi kuliko wabunge wanawake

Wabunge wanaume wanashiriki zaidi kuliko wabunge wanawake katika nyanja zote za ushiriki (mchoro 4). Hata ukichukua wabunge wanawake waliochaguliwa majimboni tu hali haibadiliki sana.

**Mchoro 4: Idadi ya ushiriki wa wabunge, kwa jinsia**




Chanzo: Tovuti ya Bunge la Tanzania ([www.bunge.go.tz](http://www.bunge.go.tz))

## Ukweli wa 6: Wabunge 72 hawajawahi kuuliza swali la msingi hata moja

Njia kuu ya kuanzisha mjadala juu ya mada fulani ni kuwasilisha maswali ya msingi. Kama mchoro namba 5 unavyoonesha, wabunge 72 hawajawahi kuuliza swali moja la msingi. Wabunge hawa wengi ni wa CCM. UDP na CUF pia wana mbunge mmoja mmoja ambao hawajawahi kuuliza swali moja la msingi.

**Mchoro 5: Wabunge ambao hawajawahi kuuliza swali la msingi, ki-chama**



Chanzo: Tovuti ya Bunge la Tanzania ([www.bunge.go.tz](http://www.bunge.go.tz))

## **Ukweli wa 7: Slaa, Msindai na Lubeleje wanaongoza kushiriki Bungeni**

Ili kubaini utendaji wa jumla wa wabunge, aina tatu za ushiriki wa wabunge Bungeni zilichanganywa na kukokotolewa ili kuweka alama za utendaji wa pekee. Mjumuisho huo ulifanyika kwa kujumlisha idadi ya awamu (ushiriki) ambao mbunge aliuliza swali la msingi au swali za nyongeza au alitoa mchango, ikimaanisha pia kwamba swali la msingi lina umuhimu sawa na swali la nyongeza na mchango uliotolewa wakati wa mjadala.

**Jedwali 1: Wabunge wenye ushiriki mkubwa zaidi**



Mhe. Dk. Wilbrod Slaa



Mhe. Mgana Msindai



Mhe. George Lubeleje

Nafasi	1	2	3
Jumla ya ushiriki	268	256	225
Maswali ya msingi	33	58	46
Maswali ya nyongeza	106	109	98
Michango	129	89	81

Chanzo: Tovuti ya Bunge la Tanzania ([www.bunge.go.tz](http://www.bunge.go.tz))

Kama mbinu hii ikitumika, Dk. Wilbrod Slaa anapata nafasi ya juu kabisa ya utendaji Bungeni kuliko wabunge wote akiwa na jumla ya ushiriki wa 268: ameuliza maswali ya msingi 33, maswali ya nyongeza 106 na michango 129. Wa pili ni Mgana Msindai akifuatiwa na George Lubeleje (Jedwali 1).

## **Ukweli wa 8: Mwinyi, Lowassa na Aziz wako mwisho katika ushiriki Bungeni**

Wabunge watatu wa kuchaguliwa hawajawahi kuchangia mijadala ya vikao hata mara moja kwa mujibu wa POLIS. Hawa ni Dk. Hussein Mwinyi, Edward Lowassa na Rostam Aziz. Kuna mbunge mwengine, Frederick Werema ambaye pia hajawahi kuchangia lakini hajawekwa kwenye Jedwali namba 2 kwa sababu aliteuliwa hivi karibuni tarehe 27 Oktoba 2009, kama Mbunge kutokana na cheo chake (Mwanasheria Mkuu wa Serikali).

**Jedwali 2: Wabunge wenye ushiriki mdogo zaidi**



Mhe. Dk. Hussein Mwinyi



Mhe. Edward Lowassa



Mhe. Rostam Aziz

Nafasi	319	319	319
Uzito wa ushiriki	0	0	0
Maswali ya msingi	0	0	0
Maswali ya nyongeza	0	0	0
Michango	0	0	0

Chanzo: Tovuti ya Bunge la Tanzania ([www.bunge.go.tz](http://www.bunge.go.tz))

### **3. Hitimisho**

Muhtasari huu umetumia taarifa zinazopatikana kwa urahisi kwenye tovuti ya Bunge la Tanzania kupima kiwango cha ushiriki wa wabunge kwenye vikao rasmi vyta Bunge. Umegundua tofauti kubwa ya viwango vyta ushiriki miongoni mwa wabunge. Ikumbukwe kwamba hiki ni kiashiria kimoja tu cha utendaji wa wabunge; wajibu mwagine muhimu wa wabunge ni pamoja na kufanyakazi kwenye kamati za Bunge na kushirikiana na wananchi kwenye majimbo yao. Hata hivyo, muhtasari huu unatoa picha muhimu kwa umma kujadili namna wabunge wanavyowakilisha maslahi ya wananchi. Pia muhtasari unatoa fursa kwa kila chama cha siasa na kila mbunge kujitathimini zaidi namna ambayo wamekuwa wakihudumia maslahi ya wananchi kwenye majimbo yao. Uwazi kwa wote na midahalo ya huru ni muhimu katika kuimarisha demokrasia na uwajibikaji nchini.

**Kiambatisho 1: Nafasi ya ushiriki wa wabunge kwenye vikao vya Bunge Tanzania (2005-2009)**

Nafasi	Jina	Jinsi	Chama	Jimbo	Aina ya Mbunge	Jumla ya Ushiriki	Maswali ya Msingi	Maswali ya Nyon-geza	Mich-ango
1	Dr. Wilbrod Peter Slaa	M	CHADEMA	Karatu	Wakuchaguliwa	268	33	106	129
2	Mgana Izumbe Msindai	M	CCM	Iramba Mashariki	Wakuchaguliwa	256	58	109	89
3	George Malima Lubeleje	M	CCM	Mpwapwa	Wakuchaguliwa	225	46	98	81
4	Diana Mkumbo Chilolo	F	CCM	Hanahana	Viti maalum	214	51	86	77
5	William Hezekia Shellukindo	M	CCM	Bumbuli	Wakuchaguliwa	208	53	68	87
6	Kabwe Zuberi Zitto	M	CHADEMA	Kigoma Kaskazini	Wakuchaguliwa	199	24	47	128
7	Godfrey Weston Zambi	M	CCM	Mbozi Mashariki	Wakuchaguliwa	192	28	57	107
8	Juma Hassan Killimbah	M	CCM	Iramba Magharibi	Wakuchaguliwa	186	22	59	105
9	Jenista Joakim Mhagama	F	CCM	Peramaho	Wakuchaguliwa	185	39	85	61
10	Susan Anselm Jerome Lyimo	F	CHADEMA	Hanahana	Viti maalum	179	21	39	119
11	Michael Lekule Laizer	M	CCM	Longido	Wakuchaguliwa	168	40	66	62
12	Lucas Lumambo Selelili	M	CCM	Nzega	Wakuchaguliwa	163	37	75	51
13	Job Yustino Ndugai	M	CCM	Kongwa	Wakuchaguliwa	161	40	74	47
14	Prof. Raphael Benedict Mwalyosi	M	CCM	Ludewa	Wakuchaguliwa	152	28	48	76
15	Mohamed Rished Abdallah	M	CCM	Pangani	Wakuchaguliwa	150	25	83	42
16	Hamad Rashid Mohamed	M	CUF	Wawi	Wakuchaguliwa	149	18	80	51
16	Said Amour Arfi	M	CHADEMA	Mpanda Kati	Wakuchaguliwa	149	23	50	76
16	Siraju Juma Kaboyonga	M	CCM	Tabora Mjini	Wakuchaguliwa	149	22	39	88
16	Esther Kabadi Nyawazwa	F	CCM	Hanahana	Viti maalum	149	27	78	44
20	Ruth Blasio Msafiri	F	CCM	Muleba Kaskazini	Wakuchaguliwa	148	28	43	77
20	Raynald Alfons Mrope	M	CCM	Masasi	Wakuchaguliwa	148	33	69	46
22	Mohamed Habib Juma Mnyaa	M	CUF	Mkanyageni	Wakuchaguliwa	144	13	58	73
22	Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya	M	CCM	Kwela	Wakuchaguliwa	144	36	70	38
22	Herbert James Mntangi	M	CCM	Muheza	Wakuchaguliwa	144	44	43	57
25	John Momose Cheyo	M	UDP	Bariadi Mashariki	Wakuchaguliwa	142	0	23	119
26	Benson Mwailugula Mpesa	M	CCM	Mbeya Mjini	Wakuchaguliwa	140	37	54	49
26	Paschal Constantine Degera	M	CCM	Kondoza kusini	Wakuchaguliwa	140	50	47	43
26	Salim Hemed Khamis	M	CUF	Chambani	Wakuchaguliwa	140	22	50	68
29	Paul Peter Kimiti	M	CCM	Sumbawanga Mjini	Wakuchaguliwa	138	35	34	69
30	Ponsiano Damiano Nyami	M	CCM	Nkasi	Wakuchaguliwa	137	32	72	33
30	James Philipo Musalika	M	CCM	Nyang'hwale	Wakuchaguliwa	137	41	76	20
32	Lucy Fidelis Owenya	F	CHADEMA	Hana	Viti maalum	135	25	36	74
33	Faida Mohamed Bakar	F	CCM	Hana	Viti maalum	131	31	74	26
34	John Paul Lwanji	M	CCM	Manyoni Magharibi	Wakuchaguliwa	129	25	24	80
35	Magdalena Hamis Sakaya	F	CUF	Hana	Viti maalum	127	20	34	73
36	Khalifa Suleiman Khalifa	M	CUF	Gando	Wakuchaguliwa	124	24	73	27
37	Stella Martin Manyanya	F	CCM	Hana	Viti maalum	120	13	21	86
37	Vita Rashid Kawawa	M	CCM	Namtumbo	Wakuchaguliwa	120	22	52	46
39	George Boniface Simbachawene	M	CCM	Kibakwe	Wakuchaguliwa	119	22	50	47

Nafasi	Jina	Jinsi	Chama	Jimbo	Aina ya Mbunge	Jumla ya Ushiriki	Maswali ya Msingi	Maswali ya Nyongeza	Michango
40	Mohamed Hamisi Missanga	M	CCM	Singida Kusini	Wakuchaguliwa	118	20	40	58
41	Emmanuel Jumanne Luhahula	M	CCM	Bukombe	Wakuchaguliwa	117	24	38	55
42	Jacob Dalali Shibili	M	CCM	Misungwi	Wakuchaguliwa	116	32	30	54
42	Hassan Chande Kigwalilo	M	CCM	Liwale	Wakuchaguliwa	116	35	50	31
44	Aloyce Bent Kimaro	M	CCM	Vunjo	Wakuchaguliwa	115	20	38	57
45	Bujiku Philip Sakila	M	CCM	Kwimba	Wakuchaguliwa	113	18	24	71
46	Hafidh Ali Tahir	M	CCM	Dimani	Wakuchaguliwa	110	22	60	28
46	Margreth Agness Mkanga	F	CCM	Hanahana	Viti maalum	110	35	23	52
46	Mwanne Ismaily Mchemba	F	CCM	Hana	Viti maalum	110	24	35	51
46	Mhonga Said Ruhwanya	F	CHADEMA	Hana	Viti maalum	107	25	33	49
50	Dr. Zainab Amir Gama	F	CCM	Kibaha	Wakuchaguliwa	106	21	49	36
50	Ernest Gakeya Mabina	M	CCM	Geita	Wakuchaguliwa	106	35	52	19
50	Aggrey Deaisile Joshua Mwanri	M	CCM	Siha	Wakuchaguliwa	106	30	34	42
50	Felix Ntibenda Kijiko	M	CCM	Muhambwe	Wakuchaguliwa	106	20	20	66
54	Mzee Ngwali Zubeir	M	CCM	Mkwajuni	Wakuchaguliwa	104	38	57	9
55	Dr. Raphael Masunga Chegeni	M	CCM	Busega	Wakuchaguliwa	103	27	50	26
56	Fuya Godwin Kimbita	M	CCM	Hai	Wakuchaguliwa	101	17	22	62
57	Castor Raphael Ligallama	M	CCM	Kilombero	Wakuchaguliwa	100	20	21	59
58	Haroub Said Masoud	M	CCM	Koani	Wakuchaguliwa	99	28	53	18
59	Mbaruk Kassim Mwandoro	M	CCM	Mkinga	Wakuchaguliwa	98	30	23	45
59	Gosbert Begumisa Blandes	M	CCM	Karagwe	Wakuchaguliwa	98	24	23	51
61	Savelina Silvanus Mwijage	F	CUF	Hana	Viti maalum	96	17	17	62
61	Stanley Jilaoneka Yono Kevela	M	CCM	Njombe Magharibi	Wakuchaguliwa	96	19	24	53
63	Ludovick John Mwananzila	M	CCM	Kalambo	Wakuchaguliwa	94	24	40	30
64	Mussa Azan Zungu	M	CCM	Ilala	Wakuchaguliwa	93	21	32	40
65	Omar Shabani Kwaang'	M	CCM	Babati Mashariki	Wakuchaguliwa	92	19	24	49
65	Martha Mosses Mlata	F	CCM	Hana	Viti maalum	92	13	25	54
67	Teddy Louise Kasella-Bantu	F	CCM	Bukene	Wakuchaguliwa	89	15	36	38
67	Jackson Muvangila Makwetta	M	CCM	Njombe Kaskazini	Wakuchaguliwa	89	21	39	29
69	Halima James Mdee	F	CHADEMA	Hana	Viti maalum	88	24	24	40
70	Peter Joseph Serukamba	M	CCM	Kigoma Mjini	Wakuchaguliwa	87	12	25	50
70	Dr. Guido Gorogolio Sigonda	M	CCM	Songwe	Wakuchaguliwa	87	18	16	53
72	Anne Kilango Malecela	F	CCM	Same Mashariki	Wakuchaguliwa	86	24	37	25
72	Yahya Kassim Issa	M	CCM	Chwaka	Wakuchaguliwa	86	28	48	10
74	Clemence Beatus Lyamba	M	CCM	Mikumi	Wakuchaguliwa	83	17	14	52
75	Ania Said Chaurembo	F	CUF	Hana	Viti maalum	82	22	26	34
75	Sijapata Fadhili Nkayamba	F	CCM	Hana	Viti maalum	82	18	24	40
77	Masolwa Cosmas Masolwa	M	CCM	Bububu	Wakuchaguliwa	81	25	16	40
77	Victor Kilasile Mwambalaswa	M	CCM	Lupa	Wakuchaguliwa	81	26	22	33
77	Mkiwa Adam Kimwanga	F	CUF	Hana	Viti maalum	81	16	18	47

Nafasi	Jina	Jinsi	Chama	Jimbo	Aina ya Mbunge	Jumla ya Ushiriki	Maswali ya Msingi	Maswali ya Nyongeza	Michango
77	Mossy Suleiman Mussa	M	CCM	Mfenesini	Wakuchaguliwa	81	42	17	22
77	Athumanzi Saidi Janguo	M	CCM	Kisarawe	Wakuchaguliwa	81	11	26	44
82	Pindi Hazara Chana	F	CCM	Hana	Viti maalum	80	21	12	47
82	Prof. Idris Ali Mtulia	M	CCM	Rufiji	Wakuchaguliwa	80	12	12	56
82	Vuai Abdallah Khamis	M	CCM	Magogoni	Wakuchaguliwa	80	14	13	53
82	Vedastusi Mathayo Manyinyi	M	CCM	Musoma Mjini	Wakuchaguliwa	80	14	21	45
82	Shoka Khamis Juma	M	CUF	Micheweni	Wakuchaguliwa	80	29	23	28
87	Estherina Julio Kilasi	F	CCM	Mbarali	Wakuchaguliwa	79	14	29	36
88	Fatma Abdallah Mikidadi	F	CCM	Hana	Viti maalum	78	11	20	47
88	James Daudi Lembeli	M	CCM	Kahama	Wakuchaguliwa	78	22	27	29
88	Mgeni Jadi Kadika	F	CUF	Hana	Viti maalum	78	23	17	38
88	Aziza Sleyum Ally	F	CCM	Hana	Viti maalum	78	21	17	40
92	Dr. Harrison George Mwakyembe	M	CCM	Kyela	Wakuchaguliwa	77	13	11	53
92	Nuru Awadhi Bafadhili	F	CUF	Hana	Viti maalum	77	13	23	41
92	Said Juma Nkumba	M	CCM	Sikonge	Wakuchaguliwa	77	30	29	18
92	Dr. Binilith Satano Mahenge	M	CCM	Makete	Wakuchaguliwa	77	13	23	41
92	Grace Sindato Kiwelu	F	CHADEMA	Hana	Viti maalum	77	11	34	32
92	Charles N. Keenja Ubungo	M	CCM	Ubungo	Wakuchaguliwa	77	18	15	44
98	Benito William Malangalila	M	CCM	Mufindi Kusini	Wakuchaguliwa	76	21	31	24
98	Ezekiel Magolyo Maige	M	CCM	Msalala	Wakuchaguliwa	76	14	26	36
100	Mwanawetu Said	F	CUF	Hana	Viti maalum	73	11	22	40
100	Janet Bina Kahama	F	CCM	Hana	Viti maalum	73	25	29	19
100	Mohammed Rajab Soud	M	CCM	Jang'ombe	Wakuchaguliwa	73	17	37	19
100	Juma Abdallah Njwayo	M	CCM	Tandahimba	Wakuchaguliwa	73	16	21	36
104	Felister Aloyce Bura	F	CCM	Hana	Viti maalum	72	10	18	44
104	Lazaro Samuel Nyalandu	M	CCM	Singida North	Wakuchaguliwa	72	18	34	20
104	Ambassador Getrude Ibengwe Mongella	F	CCM	Ukerewe	Wakuchaguliwa	72	0	25	47
104	Stephen Jones Galinoma	M	CCM	Kalenga	Wakuchaguliwa	72	17	14	41
108	Manju Salum Omar Msambya	M	CCM	Kigoma kusini	Wakuchaguliwa	71	0	31	40
108	Damas Pascal Nakei	M	CCM	Babati Magharibi	Wakuchaguliwa	71	26	16	29
108	Riziki Omar Juma	F	CUF	Hana	Viti maalum	71	17	22	32
108	Mwinchoum Abdulrahman Idd Msomi	M	CCM	Kigamboni	Wakuchaguliwa	71	18	13	40
112	Dr. Samson Ferdinand Mpanda	M	CCM	Kilwa Kaskazini	Wakuchaguliwa	70	8	18	44
112	Bakari Shamis Faki	M	CUF	Ole	Wakuchaguliwa	70	33	17	20
112	Mariam Salum Mfaki	F	CCM	Hana	Viti maalum	70	15	20	35
112	Rosemary Kasimbi Kirigini	F	CCM	Hana	Viti maalum	70	17	19	34
116	Capt. John Damiano Komba	M	CCM	Mbinga Magharibi	Wakuchaguliwa	69	16	26	27
116	Janeth Mourice Massaburi	F	CCM	Hana	Viti maalum	69	17	12	40
116	Dr. Ali Tarab Ali	M	CUF	Konde	Wakuchaguliwa	69	14	24	31
116	Daniel Nicodem Nsanzugwanko	M	CCM	Kasulu mashariki	Wakuchaguliwa	69	8	10	51

Nafasi	Jina	Jinsi	Chama	Jimbo	Aina ya Mbunge	Jumla ya Ushiriki	Maswali ya Msingi	Maswali ya Nyongeza	Michango
120	Beatrice Matumbo Shellukindo	F	CCM	Kilindi	Wakuchaguliwa	68	6	12	50
120	Dr. Luka Jelas Siyame	M	CCM	Mbozi Magharibi	Wakuchaguliwa	68	7	12	49
120	Dr. Festus Bulugu Limbu	M	CCM	Magu	Wakuchaguliwa	68	18	19	31
123	Joel Nkaya Bendera	M	CCM	Korogwe Mashariki	Wakuchaguliwa	67	16	39	12
124	Maria Ibeshi Hewa	F	CCM	Hana	Viti maalum	66	14	14	38
124	Hasnain Gulamabbas Dewji	M	CCM	Kilwa Kusini	Wakuchaguliwa	66	20	21	25
124	Ameir Ali Ameir	M	CCM	Fuoni	Wakuchaguliwa	66	10	4	52
127	Lediana Mafuru Mng'ong'o	F	CCM	Hana	Viti maalum	65	6	35	24
128	Kaika Saning'o Telele	M	CCM	Ngorongoro	Wakuchaguliwa	64	14	25	25
128	Dr. James Mnanka Wanyancha	M	CCM	Serengeti	Wakuchaguliwa	64	21	24	19
130	Zaynab Matitu Vulu	F	CCM	Hana	Viti maalum	63	6	20	37
130	Ambassador Abdi Hassan Mshangama	M	CCM	Lushoto	Wakuchaguliwa	63	19	9	35
132	Ali Said Salim	M	CUF	Ziwani	Wakuchaguliwa	62	21	31	10
132	Hamza Abdallah Mwenegoha	M	CCM	Morogoro Kusini	Wakuchaguliwa	62	9	9	44
132	Suleiman Omar Kumchaya	M	CCM	Lulindi	Wakuchaguliwa	62	15	16	31
132	Juma Said Omar	M	CUF	Mtambwe	Wakuchaguliwa	62	11	6	45
132	Martha Jachi Umbulla	F	CCM	Hana	Viti maalum	62	16	20	26
132	Philemon Ndesamburo	M	CHADEMA	Moshi Mjini	Wakuchaguliwa	62	20	17	25
138	Dorah Herial Mushi	F	CCM	Hana	Viti maalum	61	13	10	38
139	Zubeir Ali Maulid	M	CCM	Kwamtipura	Wakuchaguliwa	60	9	27	24
139	Parmukh Singh Hoogan	M	CCM	Kikwajuni	Wakuchaguliwa	60	33	21	6
139	Mtutura Abdallah Mtutura	M	CCM	Tunduru	Wakuchaguliwa	60	8	13	39
139	Masoud Abdallah Salim	M	CUF	Mtambile	Wakuchaguliwa	60	18	10	32
139	Ali Khamis Seif	M	CUF	Mkoani	Wakuchaguliwa	60	10	11	39
144	Elizabeth nkunda Batenga	F	CCM	Hana	Viti maalum	58	7	23	28
145	Ephraim Nehemia Madeje	M	CCM	Dodoma Mjini	Wakuchaguliwa	57	15	16	26
145	Dr. Charles Ogesa F. Mlingwa	M	CCM	Shinyanga Mjini	Wakuchaguliwa	57	7	9	41
145	Abdul Jabiri Marombwa	M	CCM	Kibiti	Wakuchaguliwa	57	13	11	33
145	Abdulkarim Esmail Hassan Shah	M	CCM	Mafia	Wakuchaguliwa	57	9	29	19
149	John Samwel Malecela	M	CCM	Mtera	Wakuchaguliwa	56	1	41	14
149	Christopher Olonyokie Ole-Sendeka	M	CCM	Simanjiro	Wakuchaguliwa	56	4	18	34
149	Devota Mkuwa Likokola	F	CCM	Hana	Viti maalum	56	13	24	19
152	Mwadini Abbas Jecha	M	CUF	Wete	Wakuchaguliwa	55	13	10	32
152	Hemed Mohammed Hemed	M	CUF	Chonga	Wakuchaguliwa	55	3	1	51
152	Idd Mohamed Azzan	M	CCM	Kinondoni	Wakuchaguliwa	55	7	11	37
152	Luhaga Joelson Mpina	M	CCM	Kisesa	Wakuchaguliwa	55	9	11	35
156	Richard Mganga Ndassa	M	CCM	Sumve	Wakuchaguliwa	54	17	12	25
156	Wilson Mutagaywa Masilingi	M	CCM	Muleba South	Wakuchaguliwa	54	6	6	42
156	Ramadhani Athumanli Maneno	M	CCM	Chalinze	Wakuchaguliwa	54	12	22	20
159	Gaudence Cassian Kayombo	F	CCM	Mbinga Mashariki	Wakuchaguliwa	53	9	13	31

Nafasi	Jina	Jinsi	Chama	Jimbo	Aina ya Mbunge	Jumla ya Ushiriki	Maswali ya Msingi	Maswali ya Nyongeza	Michango
159	Kilontsi Muhamma Mpologomyi	M	CCM	Kasulu Magharibi	Wakuchaguliwa	53	15	12	26
161	Cynthia Hilda Ngoye	F	CCM	Hana	Viti maalum	52	7	17	28
161	Khadija Salum Ally Al-Qassmy	F	CUF	Hana	Viti maalum	52	2	3	47
163	Zuleikha Yunus Haji	F	CCM	Hana	Viti maalum	50	12	8	30
163	Anna Richard Lupembe	F	CCM	Hana	Viti maalum	50	13	18	19
163	Dr. Diodorus Buberwa Kamala	M	CCM	Nkenge	Wakuchaguliwa	50	18	17	15
163	Fred Mpandzao Tungu	M	CCM	Kishapu	Wakuchaguliwa	50	16	10	24
167	Ibrahim Mohamed Sanya	M	CUF	MjiMkongwe	Wakuchaguliwa	49	9	18	22
167	Prof. Jumanne Abdallah Maghembe	M	CCM	Mwanga	Wakuchaguliwa	49	11	19	19
167	Maida Hamad Abdallah	F	CCM	Hana	Viti maalum	49	13	9	27
167	Dunstan Daniel Mkapa	M	CCM	Nanyumbu	Wakuchaguliwa	49	17	16	16
171	Kidawa Hamid Salehe	F	CCM	Hana	Viti maalum	48	16	15	17
171	Laus Omar Mhina	M	CCM	Korogwe Vijijini	Wakuchaguliwa	48	20	9	19
171	Prof. Philemon Mikol Sarungi	M	CCM	Rorya	Wakuchaguliwa	48	4	4	40
171	Shally Josepha Raymond	F	CCM	Hana	Viti maalum	48	6	12	30
175	Mudhahir Mohamed Mudhahir	M	CCM	Mchinga	Wakuchaguliwa	47	0	16	31
176	Dr. Omari Mzeru Nibuka	M	CCM	Morogoro Mjini	Wakuchaguliwa	46	8	8	30
177	Fatma Mussa Maghimbi	F	CUF	ChakeChake	Wakuchaguliwa	45	19	13	13
178	Bernadeta Kasabago Mushashu	F	CCM	Hana	Viti maalum	44	6	6	32
178	Josephine Johnson Genzabuke	F	CCM	Hana	Viti maalum	44	10	20	14
180	Mariam Reuben Kasembe	F	CCM	Hana	Viti maalum	43	14	13	16
181	Anastazia James Wambura	F	CCM	Hana	Viti maalum	42	7	5	30
181	Meryce Mussa Emmanuel	F	CUF	Hana	Viti maalum	42	5	14	23
183	Kheri Khatib Ameir	M	CCM	Matemwe	Wakuchaguliwa	41	11	9	21
183	Anna Maulidah Komu	F	CHADEMA	Hana	Viti maalum	41	3	6	32
185	Ahmed Ally Salum	M	CCM	Solwa	Wakuchaguliwa	40	11	16	13
185	Philip Sang'ka Marmo	M	CCM	Mbulu	Wakuchaguliwa	40	2	23	15
185	Dr. James Alex Msekela	M	CCM	Tabora Kaskazini	Wakuchaguliwa	40	8	10	22
188	Dr. Milton Makongoro Mahanga	M	CCM	Ukonga	Wakuchaguliwa	39	16	14	9
188	Eliatta Nandumpe Switi	F	CCM	Hana	Viti maalum	39	6	13	20
190	Dr. Abdallah Omar Kigoda	M	CCM	Handeni	Wakuchaguliwa	38	10	9	19
190	Charles Muguta Kajege	M	CCM	Mwibara	Wakuchaguliwa	38	6	6	26
192	Elisa David Mollel	M	CCM	Arumeru Magharibi	Wakuchaguliwa	37	11	6	20
192	Lucy Thomas Mayenga	F	CCM	Hana	Viti maalum	37	8	10	19
192	Omar Ali Mzee	M	CUF	Kiwani	Wakuchaguliwa	37	10	6	21
195	Ussi Ame Pandu	M	CCM	Mtoni	Wakuchaguliwa	36	10	6	20
196	Dr. Lucy Sawere Nyka	F	CCM	Hana	Viti maalum	35	5	9	21
196	Mohamed Said Sinani	M	CCM	Mtware Mjini	Wakuchaguliwa	35	14	7	14
196	Capt. George Huruma Mkuchika	M	CCM	Newala	Wakuchaguliwa	35	12	15	8
199	Dr. Haji Mwita Haji	M	CCM	Muyuni	Wakuchaguliwa	34	9	13	12

Nafasi	Jina	Jinsi	Chama	Jimbo	Aina ya Mbunge	Jumla ya Ushiriki	Maswali ya Msingi	Maswali ya Nyongeza	Michango
199	Brg. Gen. Hassan Athumani Ngwilizi	M	CCM	Mlalo	Wakuchaguliwa	34	5	5	24
199	Abubakar Khamis Bakary	M	CUF	B.L.W	Zanzibar HoR	34	5	7	22
202	Bernard Kamillius Membe	M	CCM	Mtama	Wakuchaguliwa	33	8	21	4
202	Eustace Osler Katagira	M	CCM	Kyerwa	Wakuchaguliwa	33	1	0	32
202	Feteh Saad Mgeni	M	CCM	Bumbwini	Wakuchaguliwa	33	7	8	18
205	Charles Mwera Nyanguru	M	CHADEMA	Tarime	Wakuchaguliwa	32	3	2	27
206	Prof. Feethan Philipo Banyikwa	M	CCM	Ngara	Wakuchaguliwa	31	11	2	18
207	Adam Kighoma Ali Malima	M	CCM	Mkuranga	Wakuchaguliwa	29	1	3	25
207	Ame Pandu Ame	M	CCM	Nungwi	Wakuchaguliwa	29	11	7	11
207	Mwaka Abdulrahman Ramadhan	F	CCM	Hana	Viti maalum	29	12	9	8
207	Mohammed Abdi Abdulaziz	M	CCM	Lindi Mjini	Wakuchaguliwa	29	10	7	12
207	Haji Juma Sereweji	M	CCM	Mwanakwerekwe	Wakuchaguliwa	29	6	8	15
207	Tatu Musa Ntimizi	F	CCM	Igalula	Wakuchaguliwa	29	6	4	19
213	Mwajuma Hassan Khamis	F	CUF	Hana	Viti maalum	28	5	0	23
214	Riziki Said Lulida	F	CCM	Hana	Viti maalum	27	5	7	15
214	Basil Pesambili Mramba	M	CCM	Rombo	Wakuchaguliwa	27	4	6	17
214	William Jonathan Kusila	M	CCM	Bahi	Wakuchaguliwa	27	6	14	7
214	Mohammed Amour Chombon	M	CCM	Magomeni	Wakuchaguliwa	27	9	9	9
218	William Mganga Ngeleja	M	CCM	Sengerema	Wakuchaguliwa	25	3	7	15
218	Ali Juma Haji	M	CCM	Chaani	Wakuchaguliwa	25	4	3	18
218	Christopher Kajoro Chiza	M	CCM	Buyungu	Wakuchaguliwa	25	0	0	25
221	Salim Abdallah Khalfan	M	CUF	Tumbe	Wakuchaguliwa	24	8	5	11
222	Bahati Ali Abeid	F	CCM	Hana	Viti maalum	23	6	4	13
222	Issa Kassim Issa	M	CCM	Mpendae	Wakuchaguliwa	23	5	5	13
222	Fatma Othman Ali	F	CCM	Hana	Viti maalum	23	6	6	11
225	Al-Shymaa John Kwegyir	F	CCM	Kuteuliwa	Presidential Nominee	22	0	4	18
225	John Magale Shibuda	M	CCM	Maswa		22	0	0	22
225	Rita Louise Mlaki	F	CCM	Kawe	Wakuchaguliwa	22	2	7	13
225	Dr. Anthony Mwandu Diallo	M	CCM	Ilemela	Wakuchaguliwa	22	0	2	20
229	Nimrod Elirehema Mkono	M	CCM	Musoma Vijijini	Wakuchaguliwa	21	1	5	15
229	Halima Omar Kimbau	F	CCM	Hana	Viti maalum	21	0	6	15
229	Samuel Mcchele Chitalilo	M	CCM	Buchosa	Wakuchaguliwa	21	8	4	9
229	Dr. Juma Alifa Ngasongwa	M	CCM	Ulanga Magharibi	Wakuchaguliwa	21	0	2	19
233	Abbas Zuberi Mtemvu	M	CCM	Temeke	Wakuchaguliwa	20	0	2	18
233	Fatma Abdulhabib Fereji	F	CUF	B.L.W	Zanzibar HoR	20	6	5	9
233	Samuel John Sitta	M	CCM	Urambo Mashariki	Wakuchaguliwa	20	0	0	20
233	Gideon Asimulike Cheyo	M	CCM	Ileje	Wakuchaguliwa	20	0	0	20
233	Sophia Mattayo Simba	F	CCM	Hana	Presidential Nominee	20	5	10	5

Nafasi	Jina	Jinsi	Chama	Jimbo	Aina ya Mbunge	Jumla ya Ushiriki	Maswali ya Msingi	Maswali ya Nyongeza	Michango
233	Mohamed Ali Said	M	CCM	Mgogoni	Wakuchaguliwa	20	11	0	9
233	Florence Essa Kyendesya	F	CCM	Hana	Viti maalum	20	2	1	17
240	Benedict Ngalamu Ole-Nangoro	M	CCM	Kiteto	Wakuchaguliwa	19	1	1	17
240	Kiumbwu Makame Mbaraka	F	CCM	Hana	Viti maalum	19	1	0	18
240	Capt. John Zefania Chiligati	M	CCM	Manyoni Mashariki	Wakuchaguliwa	19	0	0	19
240	Ahmed Mabkhut Shabiby	M	CCM	Gairo	Wakuchaguliwa	19	3	2	14
240	Rajab Ahmad Juma	M	CCM	Tumbatu	Wakuchaguliwa	19	7	2	10
245	Mwantumu Bakari Mahiza	F	CCM	Hana	Viti maalum	18	0	0	18
245	Andrew John Chenge	M	CCM	Bariadi Magharibi	Wakuchaguliwa	18	0	0	18
245	Prof. David Homeli Mwakyusa	M	CCM	Rungwe Magharibi	Wakuchaguliwa	18	8	5	5
248	Felix Christopher Mrema	M	CCM	Arusha	Wakuchaguliwa	17	1	1	15
248	Monica Ngezi Mbega	F	CCM	Iringa Mjini	Wakuchaguliwa	17	4	6	7
248	Dr. Aisha Omar Kigoda	F	CCM	Hana	Viti maalum	17	2	3	12
251	Dr. Batildan Salha Burian	F	CCM	Hana	Viti maalum	16	6	6	4
251	Dr. Rev. Getrude Rwakatare	F	CCM	Hana	Viti maalum	16	1	0	15
253	Ali Ameir Mohamed	M	CCM	Donge	Wakuchaguliwa	15	8	4	3
253	Col. Saleh Ali Farrah	M	CCM	Raha Leo	Wakuchaguliwa	15	3	3	9
253	Mwanakhamis Kassim Said	F	CCM	Hana	Viti maalum	15	6	0	9
253	Hawa Abdulrahman Ghasia	F	CCM	Mtwara Vijijiini	Wakuchaguliwa	15	0	0	15
257	Prof. Mark James Mwandosya	M	CCM	Rungwe Mashariki	Wakuchaguliwa	14	0	0	14
257	Sameer Ismail Lotto	M		Morogoro -Kusini -Mashariki	Wakuchaguliwa	14	0	2	12
257	Joyce Nhamanilo Machimu	F	CCM	Hana	Viti maalum	14	2	1	11
257	Dr. Cyril August Chami	M	CCM	Moshi Vijijiini	Wakuchaguliwa	14	0	0	14
257	Nazir Mustafa Karamagi	M	CCM	Bukoba Vijijiini	Wakuchaguliwa	14	2	4	8
262	Asha Mshimba Jecha	F	CCM	Hana	Viti maalum	13	1	0	12
262	Margaret Simwanza Sitta	F	CCM	Hana	Viti maalum	13	0	0	13
262	Joyce Martin Masunga	F	CCM	Hana	Viti maalum	13	1	2	10
262	Ambassador Hamis Suedi Kagasheki	M	CCM	Bukoba Mjini	Wakuchaguliwa	13	0	0	13
266	Anne Semamba Makinda	F	CCM	Njombe Kusini	Wakuchaguliwa	12	0	1	11
266	Dr. Maua Abeid Daftari	F	CCM	Hana	Viti maalum	12	0	0	12
266	Dr. Christine G. Ishengoma	F	CCM	Hana	Viti maalum	12	0	0	12
266	Gaudentia Mugosi Kabaka	F	CCM	Hana	Viti maalum	12	0	0	12
266	Prof. Juma Athuman Kapuya	M	CCM	Urambo Magharibi	Wakuchaguliwa	12	0	0	12
271	Thomas Apson Mwang'onda	M	CCM	Kuteuliwa	Presidential Nominee	11	0	0	11
271	Fatma Abdalla Tamim	F	CCM	B.L.W	Zanzibar HoR	11	3	1	7
271	Zabein Muhaji Mhita	M	CCM	Kondo Kaskazini	Wakuchaguliwa	11	0	2	9
271	Anna Margareth Abdallah	F	CCM	Hana	Viti maalum	11	0	1	10
271	Dr. David Mathayo David	M	CCM	Same Magharibi	Wakuchaguliwa	11	0	0	11

Nafasi	Jina	Jinsi	Chama	Jimbo	Aina ya Mbunge	Jumla ya Ushiriki	Maswali ya Msingi	Maswali ya Nyongeza	Michango
276	Dr. Mary Michael Nagu	F	CCM	Hanang	Wakuchaguliwa	10	0	0	10
276	Mohammed Gulam Dewji	M	CCM	Singida Mjini	Wakuchaguliwa	10	7	0	3
276	Suleiman Ahmed Saddiq	M	CCM	Mvomero	Wakuchaguliwa	10	0	1	9
276	Omar Yussuf Mzee	M	CCM	Kiembesamaki	Wakuchaguliwa	9	0	0	9
276	Stephen Masatu Wasira	M	CCM	Bunda	Wakuchaguliwa	9	0	0	9
276	William Vangimembe Lukuvi	M	CCM	Ismam	Wakuchaguliwa	9	0	0	9
282	Hadija Saleh Ngozi	F	CCM	Kuteuliwa	Presidential Nominee	8	2	0	6
283	Rev. Luckson Ndaga Mwanjale	M	CCM	Mbeya Vijijini	Wakuchaguliwa	7	0	2	5
283	Omar Sheha Mussa	M	CCM	Chumbuni	Wakuchaguliwa	7	0	0	7
283	Prof. Peter Mahamudu Msolla	M	CCM	Kilolo	Wakuchaguliwa	7	0	0	7
286	Joseph James Mungai	M	CCM	Mufindi Kaskazini	Wakuchaguliwa	6	0	0	6
286	Hassan Rajab Khatib	M	CCM	Amani	Wakuchaguliwa	6	0	0	6
286	Mathias Meinrad Chikawe	M	CCM	Nachingwea	Wakuchaguliwa	6	0	0	6
286	Celina Ompeshi Kombani	F	CCM	Ulanga Mashariki	Wakuchaguliwa	6	0	0	6
286	Harith Bakari Mwapachu	M	CCM	Tanga	Wakuchaguliwa	6	0	0	6
286	Abdallah Salum Sumry	M	CCM	Mpanda Magharibi	Wakuchaguliwa	6	0	0	6
286	Mustafa Haidi Mkulo	M	CCM	Kilosa	Wakuchaguliwa	6	0	0	6
286	Juma Suleiman N'hunga	M	CCM	Dole	Wakuchaguliwa	6	0	3	3
286	Lawrence Kego Masha	M	CCM	Nyamagana	Wakuchaguliwa	6	0	0	6
286	Shamsa Selengia Mwangunga	F	CCM	Hana	Viti maalum	6	2	2	2
296	Halima Mohammed Mamuya	F	CCM	Hana	Viti maalum	5	2	0	3
296	Jeremiah Solomon Sumari	M	CCM	Arumeru Mashariki	Wakuchaguliwa	5	0	0	5
296	Hezekiah Ndahani Chibulunje	M	CCM	Chilonwa	Wakuchaguliwa	5	0	0	5
296	Kingunge Ngombale-Mwiru	M	CCM	Kuteuliwa	Presidential Nominee	5	0	0	5
300	Ambassador Seif Ali Iddi	M	CCM	Kitope	Wakuchaguliwa	4	0	0	4
300	Salim Yussuf Mohamed	M	CCM	Kojani	Wakuchaguliwa	4	0	0	4
300	Dr. Emmanuel John Nchimbi	M	CUF	Songea Mjini	Wakuchaguliwa	4	0	0	4
300	Lolesia Jeremiah Bukwimba	F	CCM	Busanda	Wakuchaguliwa	4	0	0	4
300	Dr. Ibrahim Said Msabaha	M	CCM	Kibaha Vijijini	Wakuchaguliwa	4	0	0	4
300	Abdisalaam Issa Khatib	M	CCM	Makunduchi	Wakuchaguliwa	4	0	0	4
300	Oscar Rwegasira Mukasa	M	CCM	Biharamulo	Wakuchaguliwa	4	0	1	3
				Magharibi					
300	Ali Haji Ali	M	CCM	B.L.W	Zanzibar HoR	4	0	0	4
300	Col.Lt. Yusufu Makamba	M	CCM	Kuteuliwa	Presidential Nominee	4	0	0	4
309	Salum Khamis Salum	M	CCM	Meatu	Wakuchaguliwa	3	0	0	3
309	Zakia Hamdani Meghji	F	CCM	Kuteuliwa	Presidential Nominee	3	0	0	3

Nafasi	Jina	Jinsi	Chama	Jimbo	Aina ya Mbunge	Jumla ya Ushiriki	Maswali ya Msingi	Maswali ya Nyon-geza	Mich-ango
309	Mohamed Aboud Mohamed	M	CCM	Kuteuliwa	Presidential Nominee	3	0	0	3
309	Dr.John Pombe Joseph Magufuli	M	CCM	Biharamulo Mashariki	Wakuchaguliwa	3	0	0	3
313	Muhammed Seif Khatib	M	CCM	Uzini	Wakuchaguliwa	2	0	0	2
313	Ali Haroon Suleiman	M	CCM	B.LW	Zanzibar HoR	2	0	1	1
315	Mizengo Kayanza Peter Pinda	M	CCM	Mpanda Mashariki	Wakuchaguliwa	1	0	0	1
315	Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa	M	CCM	Bagamoyo	Wakuchaguliwa	1	0	0	1
317	Rostam Abdulrasul Aziz	M	CCM	Igunga	Wakuchaguliwa	0	0	0	0
317	Frederick Mwita Werema	M	CCM	Ex-officio Member	AG	0	0	0	0
317	Edward Ngoyai Lowassa	M	CCM	Monduli	Wakuchaguliwa	0	0	0	0
317	Dr. Hussein Ali Mwinyi	M	CCM	Kwahani	Wakuchaguliwa	0	0	0	0

Chanzo: Tovuti ya Bunge la Tanzania ([www.bunge.go.tz](http://www.bunge.go.tz))